

KAMATI YA SHERIA YA BUNGE LA UGANDA YAFANYA ZIARA SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Kamati ya Sheria ya Bunge la Uganda hivi karibuni imefanya ziara nchini kujifunza jinsi Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inavyofanyakazi.

Kiongozi wa wajumbe wa Kamati hiyo Mhe. Jacob Oboth alieleza kuwa ziara hiyo inalengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu wa utendajikazi hasa Baraza la maadili.

“Uganda tunataka kuifanyia marekebisho Sheria yetu ya Maadili ili tuwe na chombo chenye nguvu zaidi na kinachowajibika,” alisema.

Mhe. Oboth aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuwa na utashi wa kutunga na kusimamia sheria inayotokana na Katiba kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma.

“Katika Afrika Mashariki na hata bara zima la Afrika ukiondoa Nigeria, Tanzania ni nchi yenye Baraza la Maadili lenye nguvu linalopashwa kuigwa. Uganda tuna Baraza la Maadili, lakini halifanyikazi vizuri kama la Tanzania,” alisema.

Kwa mujibu wa Mbunge huyo, Sheria ya maadili ya Uganda haitokani na Katiba kama Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Tanzania ilivyo.

Amesema pamoja na Uganda kuwa na Sheria ya Maadili, lakini ni vigumu kumfikisha kiongozi aliyeteuliwa na Rais mbele ya Baraza hata kama ameenda kinyume na Sheria.

Kwa upande wake Kamishna wa Maadili Jaji Mstaafu Salome Kaganda amesema nguvu ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma inatokana na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 132.

“Hiki ndicho chanzo cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma,” alisema na kuongeza kuwa Sheria hiyo inatoa mamlaka ya mtu kufikishwa mbele ya Baraza la Maadili ikibainika kuwa amekiuka sheria.

Baraza la Maadili tangu lilipoteuliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2010, limeshughulikia jumla ya malalamiko 75, kati ya malalamiko hayo, 30 yalithibitika kuwa na ukiukwaji wa Maadili na viongozi husika kuchukuliwa hatua mbalimbali ikiwemo onyo, onyo kali, faini, kushushwa cheo na kuondolewa katika wadhifa.

Mpaka sasa kuna malalamiko 12 yanayosubiri kufikishwa katika Baraza la Maadili.

MWISHO